**PHILADELPHIA GAS WORKS**
800 W. MONTGOMERY AVENUE, PHILADELPHIA, PA 19122-0050

**Tarehe ya Taarifa:** {SYSTEMDATE}
**Namba ya Akaunti:** {ACCNO}

# ILANI YA SIKU 10 YA KUFUNGWA KWA GESI.
## Huenda Huduma Yako ya Gesi Ikafungwa

**Umechelewa kulipa bili yako. Kwa hivyo, PGW itafunga huduma ya gesi ya {SRVADDR} kufikia au baada ya saa 8 a.m. tarehe {DATE1}. Taarifa hii itaendelea kutumika kwa siku 60. Ili tuzungumze kuhusu bili yako au taarifa hii, piga simu kwa ofisi yetu kwa 215-235-1777.**

**Hatutafunga huduma ya gesi ukifanya MOJA ya yafuatayo:**

- Utalipa deni la bili unayodaiwa la {PAYAMT}.
- Utalipa kiasi unachodaiwa kwenye mpango wako wa hivi majuzi zaidi wa malipo.
- Utaweka mpango wa kulipa (unaweza kustahili kupokea huduma za mpango wa usaidizi maalum).
- Wasiliana nasi ikiwa unapinga bili hiyo.

**Angalau, unaweza kulazimika kulipa kiasi chote kifuatacho kabla hatujafunga huduma yako tarehe:**

| | |
|---|---|
| Deni Unalodaiwa | {PAYAMT} |
| Ada ya Ulinzi | {MONEY2} |
| Ada ya Kurejesha Huduma | {MONEY1} |
| Jumla | {MONEY4} |

**Pamoja na {MONEY3} ikiwa ni lazima tuchimbe barabara.**

**Ni jukumu lako pia kulipia huduma yote ya gesi unayopokea ambayo unapaswa kulipa sasa au ambayo umechelewa kulipa. Ikifungwa, unaweza kutakiwa kulipa zaidi ya kiasi kilichowekwa kwenye taarifa hii ili urejeshewe huduma ya gesi.**

### TAARIFA YA DHARURA YA KIMATIBABU

TUFAHAMISHE IKIWA KUNA MTU ANAYEISHI NYUMBANI KWAKO AMBAYE NI MGONJWA SANA AU NI MGONJWA. HATUTAFUNGA HUDUMA YAKO wakati wa ugonjwa huo, mradi:

1. Daktari wako mwenye leseni, msaidizi wa daktari au muuguzi anayetibu wagonjwa atathibitisha kwa maandishi kuwa ugonjwa huo upo na kuwa unaweza kuzidi ikiwa huduma yako itasimamishwa; na
2. Utaweka mpango wa kulipa bili zako za sasa.
3. Utawasiliana nasi kwa kupiga simu kwa 215-235-1777.
4. DAKTARI MWENYE LESENI, MSAIDIZI WA DAKTARI AU MUUGUZI ANAYETIBU WAGONJWA ATATUMA BARUA KWA PGW NDANI YA SIKU 3, INAYOTHIBITISHA UGONJWA HUO.

Ikiwa wewe ni mwathiriwa wa dhuluma na una amri iliyotolewa na mahakama, unaweza kupata ulinzi na taratibu maalum za matibabu ya dharura. **Tupigie simu mara moja kwa 215-235-1000 utufahamishe ili uweze kupata ulinzi na taratibu hizi maalum.** Tutahitaji utupatie nakala ya amri hiyo ya mahakama.

### JAMBO MUHIMU LA KUJUA – KABLA HATUJAFUNGA HUDUMA YAKO YA GESI

- Unaweza kustahiki kuweka makubaliano ya kulipa au kupokea huduma za mipango ya usaidizi maalum. Kujiandikisha katika mpango huu inaweza kuwa njia ya kuepuka kufungiwa huduma. Wasiliana nasi mara moja kwa 215-235-1777 ili utambue ikiwa unastahiki, na jinsi ya kujiandikisha. Tunaweza kuhitaji rekodi ya mapato yako.
- Ikiwa una maswali au unahitaji kupata maelezo zaidi, tafadhali tupigie simu leo kwa 215-235-1777 au ututumie barua katika P.O. Box 3500, Philadelphia, PA 19122. Baada ya kuzungumza na PGW, ikiwa hujaridhika, unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Tume ya Huduma za Umma ya Pennsylvania (Public Utility Commission, PUC). PUC inaweza kuchelewesha kufungwa kwa huduma ukiwasilisha malalamiko kabla ya tarehe ya kufungwa. Ili uwasiliane nao, piga simu kwa 1 (800) 692-7380 au utume barua kwa: Pennsylvania Public Utility Commission, Box 3265, Harrisburg, PA 17105-3265.
- Tupigie simu ikiwa bili yako hulipwa na mwenye nyumba. Una ulinzi fulani wa kisheria.
- Ikiwa unatatizika kuelewa au kuzungumza Kiingereza, tupigie simu ili upate huduma ya ukalimani bila malipo.
- Tafadhali wasiliana nasi ikiwa wewe ni mlemavu na unahitaji usaidizi.
- Watu wote wazima wanaoishi nyumbani, ambao majina yao yapo kwenye mkataba wa kukodisha au mkopo wa nyumba wanachukuliwa kuwa ‘mteja’ na wana jukumu la kulipa bili.
- Mtu YEYOTE mzima ambaye amekuwa akiishi nyumbani anaweza kulazimika kulipa bili yote au sehemu ya bili hii ili arejeshewe huduma.
- Huduma yako ikifungwa, lazima uwasiliane nasi baada ya kulipa ili tuhakikishe umetimiza masharti yote ya kurejeshewa huduma na tupange jinsi ya kufika nyumbani kwako. Tunaweza kuchukua hadi siku saba kukurejeshea huduma.
- Ikiwa una amri halali ya **Kulindwa Kutokana na Dhuluma** au amri iliyotolewa na mahakama inayotambulika katika Jimbo hili inayothibitisha wazi kuwa wewe ni mwathiriwa wa dhuluma za nyumbani, unaweza kupata ulinzi wa ziada. **Tupigie simu mara moja kwa 215-235-1000.** Tutahitaji utupatie nakala ya amri hiyo.

### KANUNI ZA KUFUNGWA KWA HUDUMA KATIKA MAJIRA YA BARIDI Desemba 1 hadi Machi 31

- **Wasiliana nasi kabla ya tarehe ya kufungwa kwa huduma** ili utupatie maelezo kuhusu mapato na wanaoishi nyumbani ili tuone kama unastahili kupokea huduma za mipango yoyote ya usaidizi.
- **Ikiwa mapato yako ni ya chini, kuna kanuni maalum kuhusu iwapo tunaweza kufunga huduma yako ya gesi katika majira ya baridi.** Ongeza pamoja mapato ya kila mwezi katika familia yako. Angalia chati iliyo hapa chini ili utambue kikundi chako. Tunaweza kuhitaji uthibitisho wa mapato.
- **Ikiwa mapato yako ni 150% ya mwongozo wa kitaifa wa umaskini au chini yake, lazima kwanza tuombe PUC ruhusa ya kufunga huduma yako.** Tutakufahamisha kabla hatujafunga huduma ikiwa tutaomba PUC ruhusa ya kufunga huduma ya gesi.
- **Ikiwa mapato yako yanazidi 150% lakini hayazidi 250% ya mwongozo wa kitaifa wa umaskini, hatutafunga huduma yako ikiwa moja ya masharti haya yanakuhusu:**
  - Mtu fulani nyumbani kwako ana umri wa miaka 12 au chini yake au miaka 65 au zaidi; au
  - Umelipa angalau nusu ya bili zako za gesi za miezi miwili iliyopita; au
  - Ikiwa kwa miezi miwili iliyopita umetumia angalau 15% ya mapato ya familia yako kulipa bili zako za gesi.
- **Tukikurejeshea huduma yako katika miezi ya majira ya baridi (kati ya Desemba 1 na Machi 31)** tutarejesha huduma yako ndani ya saa 24 utakapotimiza masharti yote ya kurejeshewa huduma. Tukitakiwa kuchimba barabara, tunaweza kuchukua hadi siku 7.

**Mwongozo wa Kitaifa wa Umaskini (Federal Poverty Guidelines, FPG) {FPGYR}**

| Ukubwa wa Familia | Mapato yako ni 150% ya FPG au chini yake ikiwa mapato yako ya jumla kwa mwezi ni: | Mapato yako ni kati ya 151% - 250% ya FPG ikiwa mapato yako ya jumla kwa mwezi ni: |
|---|---|---|
| 1 | {FPG1150} au chini yake | {FPG1151}-{FPG1250} |
| 2 | {FPG2150} au chini yake | {FPG2151}-{FPG2250} |
| 3 | {FPG3150} au chini yake | {FPG3151}-{FPG3250} |
| 4 | {FPG4150} au chini yake | {FPG4151}-{FPG4250} |
| Kwa kila mtu wa ziada, ongeza | {FPG5150} | {FPG5151}-{FPG5250} |

**Tafadhali turudishie sehemu hii na malipo yako.**
**Andika namba ya akaunti yako kwenye cheki yako au agizo la malipo ya kulipwa kwa Philadelphia Gas Works**

**Namba ya Akaunti:** **{ACCNO}**
**Tarehe ya Taarifa:** **{SYSTEMDATE}**
**Tafadhali Lipa:** **{PAYAMT}**

Weka "X" kwenye kisanduku cha masahihisho ya anwani. Chapisha masahihisho upande wa nyuma.

**Kiasi Kilichowekwa:**

{SoldTo}
{SoldTo2}
{SoldTo3}
{SoldTo4}
{SoldTo5}

**Philadelphia Gas Works**
**P.O. Box 11700**
**Newark, NJ 07101-4700**